

**Nyimbo:** Watu na viatu

**Mwimbaji:** Nyota Ndogo

**Video URL:** <http://www.youtube.com/watch?v=y0nKJ92DxLc>

**Maana ya maneno (words and expressions explained)**

naja (kuja) – to come

wanipokea (kupokea) – to welcome someone in

wanipa (kupa) – to give

achana nao (kuacha na wao) – leave them

husiti (kusita) – to hesitate

waniombea mungu (kuomba mungu) – to pray

chawauma (kuuma) – be in pain/hurt

ndani kwa ndani – deep inside yourself/your heart

umejisononesha (kusononeka) – be depressed/be very sad

kusonya – to hiss

sura umeikunja (kukunja sura) – to frown

waepuke (kuepuka) – to avoid

**Maswali (questions)**

1. Je, mwimbaji alikuwa akiishi vipi na rafiki yake? Eleza mambo matatu ambayo mwimbaji alikuwa akifanyiwa na rafiki yake.
2. Mwimbaji anasema kuna watu wa aina gani duniani?
3. Ni kitu gani mwimbaji alienda kumweleza rafiki yake?

4. Je, rafiki yake alionyesha hisia gani na alifanya nini?
5. Je, unafikiri Mwimbaji ana maana gani aliposema *watu na viatu*?

**Mazoezi: (exercises)**

**1. Sikiliza nyimbo halafu jaza mapengo**

Rafiki yangu \_\_\_\_\_ naja kwako siku nyingi \_\_\_\_\_ kwa uzuri siku zote

Wakati sina wanipa nitakacho husiti \_\_\_\_\_ kwako sawa waniombea

\_\_\_\_\_

Moyoni mwangu \_\_\_\_\_ nina rafiki huyu wa kweli hakuna yule ambaye

\_\_\_\_\_ kati yetu

**Kiitikio:**

Ooo kuna watu na viatu \_\_\_\_\_

Ooo kuna watu wasiopenda \_\_\_\_\_

Ooo ukiwa nacho chawauma \_\_\_\_\_

achana nao waepuke haraka sana

Hivi majuzi nilipata \_\_\_\_\_ \_\_\_\_\_ nikaja kukueleza

Mtu wa \_\_\_\_\_ nilifikiria ni wewe rafiki yangu

Nilifurahi na \_\_\_\_\_ na kutaja jina lake mungu

Nikikuangalia mwako \_\_\_\_\_ umejisononesha

Ukaanza \_\_\_\_\_ ukirusha mikono sura umeikunja kumbe \_\_\_\_\_

mafanikio yangu ilikuwa hatia mimi kuja kukueleza x 2

Mtu wa kwanza mimi kumfikiria ni we rafiki yangu

2. Eleza kwa kifupi nyimbo hii inazungumzia nini?
3. Unafikiri kisa cha nyimbo hii kinaweza kutokea hapa Marekani? Kwanini?
4. Tayarisha mchezo wa kuigiza juu ya nyimbo hii.
5. Andika sentensi zenye maana kwa kutumia maneno haya:
  - i. Kuepuka
  - ii. Mpendwa
  - iii. Kuomba mungu
  - iv. Kusononeka
  - v. Kusita